MALEZI KATIKA UISLAMU

Na

Abdulla Talib Abdulla

Utangulizi

Sifa njema zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mlezi aliemuumba mwanadamu, akampa akili na baadhi ya utambuzi kisha akamfadhilisha kuliko viumbe vyake vingi; na wakati mwengine akamshusha chini kuliko walio chini. Sala na salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad SAW aliesema**: *"Bila shaka nimetumwa kuja kukamilisha misingi ya tabia njema*"**. Mwenyezi Mungu amrehemu pamoja na masahaba zake na wafuasi wake wanaoyakinisha kuwa mpaka siku ya kiama. Ama baada ya hayo.

Bila shaka Uislamu ni dini inayotoa uhuru mkubwa kwa mwanadamu. Mara nyingi mtu huchagua na kuamua kwa uangalifu mkubwa jambo ambalo litamletea manufaa zaidi yeye mwenyewe na wenzake anaowatakia kheri. Uhuru hauna maana ya kushibisha matamanio ya nafsi tu wala kufanya upendalo - kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu ***((Kwa hakika ya nafsi ni yenye kuamrisha sana maovu))*** Quran 12:53. Uhuru ndio uliomtofautisha mwanadamu na malaika. Mwanadamu alipewa uhuru wa kuamini au kukufuru, kuwa mwema au muovu na hata kufanya maamuzi ya lengo kuu la kuumbwa ambalo ni kuamua hatma ya maisha ya milele ima yakawe peponi au yakawe motoni. Mwenyezi Mungu anasema ***((Na (naapa) kwa nafsi na kwa aliyeitengeneza. Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake. Bila shaka amefaulu aliyeitakasa (nafsi yake) Na bila shaka amehasirika aliyeiviza))*** Quran 91:7-10.

Malezi yana nafasi kubwa katika kumtengeneza mja aweze kutumia uhuru wake vizuri. Tunapoliangalia neno malezi katika uislamu tutalikuta lina vipengele vinne vikubwa vya:-

i). Kuhifadhi maumbile (fitra) ya kinachokulia na kukiendeleza;
ii).Kukuza vipaji na kuviendeleza;
iii).Kuyaongoza mambo ya kimaumbile na vipaji hivyo kwendea katika wema; na
iv) Kwenda kwa tadaruji katika kufikia malengo.

Aidha Mlezi anapaswa kutambua mambo yafuatayo ambayo ndio msingi wa malezi:-
i). Malezi ni lazima yawe na malengo, mikakati na shughuli.
ii).Mlezi Mkuu ni mwenyezi Mungu ambae ndio Muumbaji wa Maumbile na Mtoaji wa vipaji na Muwekaji wa sheria na taratibu.
iii)Malezi ni lazima yawe na mpango maalumu unaokwenda hatua kwa hatua.
iv)Kazi ya mlezi inapaswa ifuate program aliyoiweka Mwenyezi Mungu katika Ulimwengu.

Kujisalimisha katika matakwa na sheria za Allah ndio msingi na lengo kuu la malezi katika uislamu. Kujisalimisha huko ndiko kunakoikomboa akili, moyo na tabia kutokana na utumwa wa maisha ya dunia na athari za maovu yote. ***((Ambao wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiyejua kusoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anayewaamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na anawaharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao. Basi wale waliomuamini yeye, na wakamheshimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.Quran))*** Quran 7:157.

MAREJEO YA MALEZI KATIKA UISLAMU

Malezi ya kiislamu ni kuijenga nafsi ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla iweze kuukumbatia Uislamu na kuutekeleza kwa ukamilifu katika maisha yake yote. Kwa msingi huo marejeo yale yale ya uislamu yaani kitabu na Sunna ndio marejeo ya Malezi katika uislamu.

Wakati Mwenyezi Mungu alipomuumba baba yetu Adam AS; malaika kwa elimu waliyopewa walimuona ((***atakaefanya uharibifu humo na kumwaga damu***)) lakini mwenyezi Mungu akajibu kuwa ((***Hakika Mimi nayajua msiyoyajua***))***;*** kwa maana hiyo akatoa utambuzi mtakatifu wa kiumbe hiki cha kipekee na akakiri kuwa uhuru unaweza kumpelekea katika ufisadi. Hii ni kwa nini? Kinyume na itikadi ya wengi, Uislamu umetangaza kuwa hakuna kulazimishana katika kuamini lakini mtu atahesabiwa na kulipwa kwa uamuzi na uchaguzi wake wa imani. Anasema ((***Hapana kulazimisha katika (kufuata) Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Huwatoa gizani na kuwaingiza mwangazani. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni Mashet'ani. Huwatoa kwenye mwangaza na kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu (Milele).))*** Quran 2:256-257.

Uislamu unaifananisha jamii na jahazi iliyobeba abiria kwenye bahari kuu. Kila mmoja huwa na jukumu la kuilinda na kuihifadhi jahazi ile kwa sababu lolote litakaloitokea jahazi ile ikazama basi wote watazama na mali zao kupotea. Mtume SAW katika kuelezea wajibu huu wa pamoja amesema: ***"Mfano wa watu waliosimama katika mipaka ya Allah na wenye kuikiuka ni sawa na watu wanaosafiri pamoja katika jahazi. Ikawa baadhi yao wako katika tabaka ya juu na wengine wako tabaka ya chini. Ikawa wale walioko chini wakitaka maji wanapanda juu. Wale walioko juu wakawaambia: hatutokuruhusuni kuchota maji (huku juu) kwa sababu mnatukera. Kwa kujibu hilo walioko chini wakasema tunaweza kutoboa tundu katika jahazi (kwenye tabaka yetu ya) chini hivyo hatutowakera walioko juu. Katika hali hii, iwapo (wa juu) watawawacha (wa chini) wafanye wapendavyo basi wote wataangamia na kama watawashika mkono (kuwakanya na kuwasaidia) basi wataokoka wote)).***

MSINGI WA FIKRA KATIKA MALEZI YA KIISLAMU

Uislamu unashajiisha uhuru wa kufikiri ili kujenga tabia madhubuti na misimamo usiyoyumba. Hii inatokana na kuwa elimu na uhakika unatokana na kujiamini. Mtume (S.A.W) ametuasa tusiwe wenye kuiga tu au kufuata wanayoyasema na kuyatenda watu wengine. Amemtaka mtu akuze kipawa chake cha

kufikiri ili aweze kutoa maoni yake yatakayojengeka kwa mfumo wa kiislamu. Mtume (S.A.W) anasema ***" Asiwe mmoja wenu mfuataji ((mwigo) tu anasema. Mimi nipo pamoja na watu iwapo watu watafanya vizuri nami nitafanya vizuri na iwapo watafanya vibaya nami nipo nao. Lakini jimakinisheni ili watu wakifanya mazuri nanyi mfanye na wakifanya uovu mjiepushe nao."***

Uislamu unalazimisha mtu aseme ukweli katika kutekeleza kwake uhuru wa kujieleza na kutoa maoni. Hata hivyo, uislamu umeweka baadhi ya vizuizi katika uhuru wa maoni na kujieleza pamoja na kuheshimu sana uhuru huo. Vizuizi hivi vinalenga uhuru huo utumike vizuri kwa kuzingatia ridhaa ya Mwenyezi Mungu na maslahi ya jamii na mtummmoja mmoja. Miongoni mwa vizuizi hivyo ni kuwa kujieleza na kutoa maoni ni lazima kuwe kwa njia za amani na kusimama kwa nguvu ya hoja na sio hoja ya nguvu. Maoni au kujieleza ambako kutahatarisha amani ya wanajamii au kuondoa heshima zao kunakatazwa katika dini Mwenyezi Mungu anasema***:((Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao,huenda wakawa ni bora kuliko wao. Wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane heshima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha kuamini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu. Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anayependa kula nyama ya nduguye aliyekufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu. Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume (mmoja) na mwanamke (Mmoja). Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.)***)Quran 49:11-13.

Mtume SAW amesema: ***"Mwenyezi Mungu Mtukufu amefaradhisha baadhi ya mambo basi msiyapuuze; Na akaweka mipaka (katika baadhi ya mambo) basi msiikiuke; Na akakataza baadhi ya mambo basi msiyaingie; na akayanyamazia baadhi ya mambo ikiwa ni rehma kwenu sio kwamba ameyasahau basi msiyapekuwe".*** Tunatakiwa kuwa na fikra za udadisi (*critical thinking*) na fikra za ubunifu (*creative thinking*) ili tuweze kuwa katika nafasi ya kufanya uchaguzi sahihi wa mambo yetu yote na baadae kuyaendeleza kiudhati na kwa bidii kubwa. Ni lazima tuhakikishe kuwa tunashinda changamoto na matatizo yanayotukabili baada ya kuyatafakari vyema kwa kuzingatia hali halisi inayotuzunguka na mahitaji ya zama tulizonazo. Tuweke mikakati kwa kuzingatia uhuru tulionao; tupime uwajibikaji kwa taratibu tulizojiwekea na tujijengee tabia ya kujikagua na kujihakiki wqenyewe kabla ya kuhesabiwa na kuhakikiwa na waliotupa dhamana na mwishowe kwa Muumba wetu.

Sifa za Mlezi Muislamu

Ili Mlezi aweze kutimiza wajibu wake ni lazima afungamane na sifa njema zifuatazo:-

1. Lengo, tabia na fikra zake ziwe zimefungamana na Mwenyezi Mungu. Amesema Mtukufu: ***((Haiwezi kuwa mtu aliye pewa na Allah Kitabu na hikima na Unabii kisha awaambie watu: Kuweni wa kuniabudu mimi badala ya Allah. Bali atawaambia: Kuweni wenye kumuabudu Mola Mlezi wa viumbe vyote, kwa kuwa nyinyi mnafundisha Kitabu na kwa kuwa mnakisoma))*** Quran 3 :79

2.Awe na ikhlasi katika kazi yake kwa kutarajia kupata radhi za Mwenyezi Mungu.
3. Awe ni mwenye subira katika katika kukabiliana na mitihani mbali mbali katika shughuli za ulezi. Amesema Mtukufu : ***((Naapa kwa Zama! Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara,lla wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri))*** Asr 1-3.
4. Awe mkweli wa anayoyafundisha. Amesema Mtukufu: ***((Enyi mlioamini! Kwa nini mnasema msiyo yatenda? Yanachukiza mno kwa Mwenyezi Mungu kuwa mnasema msiyoyatenda.))*** Saaf 2-3.
5. Awe daima ni mwenye kupenda kujifunza mambo mapya na yanayohitajika.
6. Awe ni muadilifu.

HALI HALISI KIMALEZI VISIWANI MWETU

Ndugu walezi, tunapoangalia maendeleo ya visiwa vyetu, tunaona vyuo na misikiti inajengwa na kuimarishwa katika kila pembe, mavazi ya kiislamu yanavaliwa na vijana na wazee waliowengi, watoto na vijana wengi, kike kwa kiume, wamekuwa wanahifadhi Quran, Mwamko wa kiislamu umekuwa unaongezeka, kazi za kuamrishana mema na kukatazana maovu zimekuwa zikiendelezwa na mtu mmoja mmoja na makundi mijini na vijijini. Kwa upande mwengine, harakati za elimu zimekuwa mno katika fani zote tokea za Quran, hadith, itikadi, sharia, historia, lugha n.k vitabu vyake mashuhuri vinapatikana na Tulabul-ilmu, wamejikusanyia fani hekma na maarifa kutoka humu humu mwetu na kila pembe ya dunia,

Pamoja na maelezo hayo bado mmporomoko wa maadili nao umezidi kwa kiasi kikubwa. Pamoja na kukua elimu lakini pana upungufu mkubwa wa *"maulamaa rabaniyun*". Ni ukweli usiopingika kuwa katika wakati wetu huu, kumekuwa na wasemaji wengi sana wanaozungumzia mambo ya kiislamu, tokea ya msingi (*usuli),* hadi mambo madogo madogo (*fur-uu*) ambayo yanahitaji elimu ya kina na hikma kubwa, hali ya kuwa wao sio Ahlu wa ilmu. Na kila mzungumzaji hupata wasikilizaji, mashabiki na hata waenezaji na wenye kuyanusuru maneno hayo. Hali hii imeleta mtafaruku mkubwa baina yetu, ikazaa migongano na hatimae makundi yenye kupingana.Tukaanza kumtafuta mchawi anaetuponza hali ya kuwa chanzo ni sisi wenyewe, kama alivyosema Imamu Shafii katika shairi lake *La nuibu zamanina wal-aybu fiyna* ambayo tafsiri yake ni*"Tunautia aibu wakati wetu hali ya kuwa aibu tunazo sisi wenyewe, wala hauna wakati aibu isipokuwa ni sisi wenyewe. Na tunausingizia wakati wetu wala hauna dhambi. Na lau kama wakati unazungumza basi ungetusuta. Na mbwa mwitu katu hali nyama ya mbwa mwenzake lakini sisi tunakulana wenyewe kwa wenyewe – dhahiri shahiri".*

Tunatakiwe tuwe na hadhari kubwa kuhusiana na wapi tunachukuwa Dini yetu. Tutambue kuwa Mtume Muhammad (SAW) alituhadharisha kuwa watakuja walinganiaji katika milango ya Jahannamu na atakaewajibu watamtumbukiza motoni. Na akawabainisha kwa kusema ***"Ni watu walio katika ngozi yetu (yaani waislamu), na wanazumgumza kwa ndimi zetu (kitabu na Sunna)".*** Hivyo ni lazima tuhakikishe kuwa anaezungumzia Dini huwa hasemi kwa matamanio ya nafsi yake. Bali huwa anabainisha hukmu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika jambo analolizungumza. Na hii ndio sababu iliyompelekea Imamu Ibnu-l-Qaym kuwaita wanachuoni kuwa ni watia sahihi(*signatory)* kwa niaba ya Mwenyezi Mungu katika kitabu chake maarufu cha *iilamul Muwaqiina an rabbil-aalamiin*.

Hivyo tujuwe kuwa kutoa fatwa na kuzungumzia masuala ya Dini sio jambo jepesi hata kidogo. Ndio maana masahaba na maulamaa wema waliopita, pamoja na kuwa walikuwa na ilmu nyingi na uzoefu mkubwa na mambo ya Dini, lakini kila mmoja alipendelea zaidi salama kwa kukaa kimya ili mwenzake ndie azungumze. Kama ilivyopokelewa kutoka kwa Abdulrahmani Bin Abilaylah aliposema: *"Hakika nimewakuta katika msikiti huu masahaba wa kiaswari 120 na hakuna yeyote miongoni mwao anaezungumzia hadithi ila hupendelea lau kama nduguye angelimtosheleza kwa hadithi hiyo, wala haulizwi suala ila hupendelea lau kama nduguye angelimtosheleza kulijibu"*

Tatambuwe kuwa kuzungumzia chochote katika Dini au kutoa FATWA katika masuala ya kisheria pasipokuwa na ilmu nayo ni miongoni mwa madhambi makubwa yenye kuangamiza. Amesema Mwenyezi Mungu *((Sema, Mola wangu ameharamisha mambo machafu yaliyodhihirika na yaliyofichika, na dhambi ,na kutoka katika utiifu pasipo haki, na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ambacho hakukiteremshia dalili,* ***na kusema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua****)).* Ameyakamilisha mambo haya matano yaliyoharamu kwa kuzungumza kuhusiana na Allah katika yale usiyoyajua. Na hii imeingia kuzungumzia dhati ya Mwenyezi Mungu, Sifa zake, mas-ala ya kadhaa wal kadar, ibada na mambo yote ya kisheria.

MALEZI YA VIJANA

Umri wa ujana unahitaji usimamizi, ulinzi na maelekezo imara kwani ndio kipindi kinachoamua mustakbali wake kwa hivyo kijana inabidi asawazishwe kwa hekina kubwa sio kwa adhabu na vitisho.Amesema Mtume SAW ***Chezeni nao miaka saba, wafunzeni miaka saba na wafanyeni marafiki miaka saba."*** Vijana ndio viongozi na walezi wa kesho na kadiri tutakavyowalea na kuwaongoza ndiyo kizazi kijacho kitakavyokuwa chema . Amesema Sayyidna Omar akiusia kuwaandaa vyema vijana ***"... kwani wao wameumbwa kwa kizazi sio kizazi chenu na zama sio zama zenu"***

Vijana wamejaa ari, hamasa, ushujaa, nguvu na vipaji vikubwa kabisa. Mwenyezi Mungu ameashiria hayo aliposema: Alkahfi:13 ***"Hao ni vijana waliomuamini Mola wao nasi tukawazidishia uongofu".*** Maadui wanatumia gharama kubwa na silaha za kisasa ili fikra na maadili ya vijana yawafuate wao kwani wanajua ulaini wa nyoyo zao hivyo wanapandikiza ili watutawale .Kwa hili Mtume ameelekeza ***"walazimuni watoto wenu na zifanyeni njema adabu zao "*** Hivyo msingi wa adabu nzuri ni kijana kuinukia katika misingi ya Uislamu kidini Mtume (S.A.W) amesema ***"Hakika nimetumwa kukamilisha tabia njema".***

Sifa za kjana bora ambae tunapaswa kumuandaa ni yule:-

- Mwenye elimu, hekma na busara.
- Mwenye kumshukuru Allah na kuwathamini jamaa na wanadamu wenzake
- Alieandaliwa vyema ili aweze kuendeleza mazuri yalikapofikia.
- Alie muadilifu, mcha mungu na mwenye kuusimamia uadilifu na haki.
- Awe ni mwenye kuthamini na kukiri juhudi na fadhila za waliomtangulia.
- Msamehevu na mwenye kuchunga hali, dharura na mazingira yanavyokwenda.
- Mwenye kuhakiki taarifa anazopelekewa nakuzifanyia kazi.

- Mwenye dira na anaejiamini katika kutoa maamuzi.

MISINGI YA KULEA FAMILIA NA KUTATUA MIZOZO YAKE

Maisha ya kifamilia ndio msingi mkuu wa jamii ya kiislamu. Chimbuko la maisha ya kifamilia linarejea tokea kuumbwa kwa mwanadamu wa kwanza. Mwenyezi Mungu anasema***:((Enyi watu, mcheni mola wenu aliyekuumbeni kutokana na nafsi moja; na kutokana na nafsi hiyo akaumba mkewe na kwa wawili hao akaeneza wanaume wengi na wanawake)) {Nisaa:1}***. Kwa maana hiyo familia ni taasisi iiliyoanzishwa na mwenyewe Mwenyezi Mungu.

Ndoa ndio asili ya familia katika uislamu. Jamii njema inaweza kujengeka pale tu mwanamme na mwanamke watashikamana kwa msingi madhubuti ulitokana na mkataba wa ndoa unaoridhiwa na dini. Ndoa hujenga mapenzi, kusaidiana, kuhudumiana na kushirikiana baina ya mume na mke. Aidha, inajenga amani na utulivu wa nafsi na kutoa mazingira mazuri ya kuandaa na kukuza kizazi chema kwa maslahi ya jamii nzima.

Jamii ya kiislamu imejengeka kwa utiifu na kujisalimisha kwa Muumba. Mume na mke waliooana wote ni waja wa Mwenyezi Mungu na ni makhalifa wake katika ardhi. Kwa maana hiyo ndoa isije ikawa ni kikwazo cha kupatikana lengo la maisha na radhi za Allah na Mtume wake. Kinachotakiwa ndoa iwe ni kituo cha awali cha kuleana na kuandaa kizazi kipya.

Tafiti nyingi zilizofanyika hapa Zanzibar zinaonyesha kuwa talaka zimekuwa zikiongezeka miongoni mwa wanandoa na wajibu wa ndoa umekuwa hauzingatiwi na mara nyingi hupelekea wanawake na watoto kunyanyasika kabla, ndani na baada ya ndoa. Hatma ya haya ni jamii nzima kuparaganyika. Miongoni mwa sababu kuu ya kuvunjia ndoa ni talaka inayosababishwa na kutelekezwa mke kwa muda mrefu bila ya kupata huduma za msingi; kuingia ndani ya ndoa bila ya kuelewa hasa dhima ya ndoa: mizozo na kutokuelewana inayochochewa na mabadiliko ya maisha kiuchumi, kijamii, kimaadili na kiutamaduni.

Ili mafungamano hayo yalete tija na malengo yaliyokusudiwa, ni vyema kila mmoja kati ya bwana na bibi akajua haki na majukumu yake na wakashirikiana na kusaidiana katika msingi wa mahaba na huruma ili maisha yao yawe mazuri na yenye kuridhiana ndani yake.Amesema Mwenyezi Mungu akibainisha haki hizo *((**Na wao wanawake wana haki juu ya waume zao mfano wa (yale majukumu yaliyo juu yao) na wanaume wana daraja kwao**)) Baqara:228* . Huu ndio msingi wa haki na wajibu katika ndoa ya kiislamu. Aidha inatupasa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Utu wa mwanamme ni sawa na utu wa mwanamke.
- Mwanamme ni mwenye kumhitaji mwanamke ili kukamilisha utu wake, kama ambavyo mwanamke ni mwenye kumhitaji mwanamme; hivyo mmoja wao hakamiliki ili kwa kumpata mwenzake.
- Umbile la mwanamme na mwanamke yako tofauti, hivyo ni lazima washirikiane na kusaidiana ili kila mmoja atumie vyema kipawa alichonacho kwa mujibu wa maumbile yake, na amsaidie mwenzake katika mapungufu aliyonayo kwa mujibu wa maumbile

- Kila mmoja kati ya mume na mke yuko huru na anayo haki ya kuwa na mawazo yake binafsi, kufuata mawazo ya mtu au kundi jengine lolote kwa kutumia kipawa cha elimu na akili aliyopewa na Allah ili atofautishe baina ya haki na batili, zuri na baya , lenye maslahi na lenye madhara.
- Mwanamke anayo haki ya kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika; pia kuizalisha mali yake kwa njia za halali kama alivyokuwa nayo mwanamme haki hiyo. Aidha kila mmoja wao ana haki ya kutumia mali yake apendavyo kama kwa sadaka, zaka, zawadi n.k ili mradi tu jambo hilo ni halali.
- Mwanamke anayo haki ya kushiriki kaitka harakati za kijamii zinazohusiana na dini , siasa, elimu, uchumi, maendeleo na ustawi kama alivyo mwanamme madhali sheria nyenginezo hatozivunja.
- Watoto wanatakiwa kupatiwa malezi mema ili waondokee kuwa ni waumini wazuri bila ya kubaguliwa baina ya wanaume na wanawake au kupendelewa.
- Mwanamme na mwanamke wote wako sawa mbele ya sharia, hivyo kila mmoja anapata haki na analazimika kutekeleza majukumu yake ya kisharia; na pia kuvitumia vyombo vya kisheria kudai haki yake yoyote kutoka kwa chombo au mtu yoyote ambazo anahisi amedhulumiwa.
- Talaka ni halali inayomchukiza Allah, hivyo ni vyema pande mbili zikafikiria vyema kabla ya kuitoa au kuidai. Aidha ni jambo ambalo halitaki mash-khara kwani ukweli wake na mas khara yake huwa inatuka. Hivyo ni vyema kunapotokea kutokuelewana wajaribu kusahihishana kwa mazungumzo, kuita wapatanishi kufanya sulhu n.k. kabla ya kuamua kuachana.
- Talaka ya inapotamkwa, huanza kuchukuliwa hukumu yake mara tu baada ya kutamkwa, wakati talaka ya kuandikwa huanza athari yake mara tu baada ya mtalikiwa kuisoma. Katika kipindi chote cha eda mume atalazimika kumhudumia mtalikiwa. Aidha mtaliki ndie atakaelazimika kuisajili talaka na kulipia gharama hizo zake kama anavyolipia cheti cha ndoa.

Kutatua Mizozo inapowashinda wanandoa wenyewe

Ni jambo lililothibiti kuwa kutokuelewana kokote kwa watu wanaopendana kama mke na mume kunatakiwa kushughulikiwa na kusuluhishwe kwa siri kabisa na wanandoa wenyewe bila ya kumshirikisha mtu mwengine yeyote. Hali hii hujenga mapenzi zaidi, kusameheana na kuhurumiana baina yao, kupunguza kujenga misimamo ya kiushindani na hata kuzuwia fitna kutoka nje ya wanandoa. Iwapo wanandoa watashindwa kutatua kutokuelewana kwao basi bado njia za mazungumzo zinatakiwa kuendelea kwa kuipeleka kadhia katika ngazi ya familia. Anasema Mtukufu ***((Na kama mkijua kuna ugomvi baina ya mke na mume basi pelekeni mwamuzi mmoja katika jamaa za mwanamme na mmoja katika jamaa za mwanamke. Kama wakitaka mapatano mwenyezi mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa habari za siri na habari za dhahiri))*** *{An-nisaa:35}.*

Hapa inakusudiwa watu wema na wenye hekma kutoka upande wa mwanamke na mwanamme ili wasaidie kuwaongoza wanandoa kufikia katika maelewano. Watu hawa wanatakiwa watoke katika familia za wanandoa lakini pia anaweza kushirikishwa rafiki iwapo ni mwenye hekma, uchamungu au/na nguvu zinazofanana na mzee. Utaratibu unaotakiwa kufuatwa ni kuwa watu wawili watoke katika pande mbili ili kila mmoja apate uwakilishi anaouridhia. Watu hawa watateuliwa ili waangalie kwa pamoja vyanzo vya

mivutano na matokeo yake ili waweze kutoa suluhisho bora kabisa la kusitisha mivutano na kujenga misingi ya mahusiano mema ya kindoa.

Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuweka watu makhsusi ili kutoa uhuru kamili kwa familia kupendekeza mtu wanaemuafiki zaidi kushiriki katika usuluhishi huu. Cha kuzingatia ni kuwa Mwenyezi Mungu ameashiria kuwa wasuluhishi hawa wanaweza kuwa sababu kubwa ya kutengamaa au kuvunjika kwa ndoa kwa kuzingatia nia na makusudio yao. Anasema Mtukufu *((Iwapo watataka islaha basi Mwenyezi atawafikisha baina yao)).* Historia inaonyesha kuwa mizozo ya ndoa ilipokuwa inapelekwa katika mahkama za kiislamu, makadhi wakibaini kuwa hatua hii haikupitiwa basi makadhi walichukua mamlaka ya kuteua wawakilishi wa pande mbili ili walisuluhishe nje ya mahkama kabla makadhi hawajakaa na kulihukumu kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa madhehebu ya Imam Shafi na Abu Hanifa makubaliano na hukumu ya wasuluhishi haiwalazimikii wanandoa kuifuata. Wanachotakiwa kufanya ni kupendekeza njia zinazoongoza kuelekea kwenye mapatano na suluhisho endelevu. Mume na mke bado watakuwa na haki ya kukubaliana au kuyakataa mapendekezo ya wasuluhishi. Hata hivyo, iwapo wana ndoa wamewawakilisha wasuluhishi kutoa uamuzi wowote kwa niaba yao, hapo watafungika na maamuzi yoyote yatakayotolewa sawa kama maamuzi hayo ni kuendelea na ndoa kwa masharti maalum au bila ya masharti; kuvunjwa ndoa kwa talaka au kuvunjwa kwa *khuluu* (talaka inayoanzishwa na mke).

Mara nyingi watu hufikia maamuzi ya kuvunja ndoa zao kwa sababu kuna mengi huwa hawayafikirii. Baya zaidi ni pale inapobakia talaka moja na ikisha kutolewa wote wawili hujuta nakuanza kutafuta fatwa itakayowarejesha. Ama wanaotafuta wasuluhishi, mara nyingi baada ya vikao kadhaa hufikia muafaka na kurejea katika ndoa na pengine ikiwa bora zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Msuluhishi anatakiwa asikilize pande zote mbili ili aweze kuwaongoza wanandoa na kujua kiini cha tatizo. Anatakiwa alisogeze tatizo karibu mno ili aweze kuona vichocheo vyote vilivyomo vikubwa na vidogo. Mara nyingi panapokuwa na kutokuelewana, wahusika huwa hawataki kuwasikiliza wale wanaozozana nao. Aidha hujenga misimamo ya nini atakisema au atakifanya kabla ya kufika katika mazungumzo. Hivyo msuluhishi ni lazima achekeche vyema na atumie hekma ili kujua kile hasa kinachobishaniwa na kutakiwa na kila upande. Akilimudu hili, msuluhishi atakuwa amepiga hatua kubwa kabisa katika kazi yake.

Msuluhishi anatakiwa kuwa mvumilivu sana kwani unapoanza kusuluhisha mara nyengine ghadhabu za pande zote mbili zinaweza kukuelekea wewe. Aidha pamoja na nia yako njema na kujitahidi kufanya uadilifu unaweza kushushiwa tuhuma nzito na unaowasuluhisha au mtu wa tatu ambae ana matakwa na mahitaji fulani katika mzozo ule. Msuluhishi anatakiwa awe msikivu mzuri na ajitahidi asiwe msemaji sana; pia aweze kumudu kukaa muda wote wa kikao na achague muda ambao atakuwa na nafasi ya kutosha na sio kuharakia harakia.

Ni kweli kuwa sio mara zote msuluhishi anafaulu kupata suluhisho bora lakini kadiri anavyojiandaa vyema ndivyo anavyowawezesha wanandoa kufikia hatua ya juu kabisa ya mapatano yenye maslahi yaliyo awla. Kwa vile waislamu ni umma mmoja wanavyoni au maimamu wanaweza kuchukua nafasi ya wazee pale ambapo kwa namna moja au nyengine wazee hawakutekeleza wajibu wao wa usuluhishi na pengine mume na mke wamefikia daraja la kutokukubaliana kwa lolote hata kuleta usuluhishi.

Inadhihirika kuwa mara nyingi usuluhishi ndio njia bora ya kutatua mizozo ya kifamilia na pale inaposhindikana tu na kukawa hapana uwezekano wa kuleta suluhu ndio kupelekwa mahakamani. Kimsingi maisha ya ndoa yamejengeka kwa mapenzi na kuhurumiana; katika mazungumzo ipo nafasi kubwa kabisa ya kukumbusha na kuraghibisha katika mapenzi. Ama upande wa sheria, mahkama inachoangalia na sheria inasemaje? Wakati mwengine mtu mwenye mantiki na fasaha ya kusema anaweza akahukumiwa kupatahaki hata kama hastahiki.

Cha kujiuliza jee hukmu zote zinazotolewa na mahkama ya kadhi zinatekelezeka? Iwapo mume au mke hamtaki mwenzake na kadhi akahukumu wabakie kama mke na mume kwa kuzingatia sheria bila ya kuziraghibisha nafsi na kuzichunga chunga ili ziridhie hilo nini kinachotarajiwa? Wengapi wamewafanyia visa wenzao kwa hukumu kama hizi?

XXXXXXXXMiongozo na hatua za kulea msuluhishi wa mizozo ya kifamilia.

Mlezi, Mzee, mwanachuoni, kiongozi wa dini, Imam na mwalimu (ustadh) ana dhamana kubwa katika jamii ya kiislamu. Iwapo atakuwa muadilifu wa kikweli atakuta kuwa wengi watamwendea ili awasaidie kutatua mizozo ya kifamilia. Nyumba ni kunga, hata kama moshi hauonekani lakini familia nyingi katika jamii yetu zina matatizo mengi ambayo yanahitajia usuluhishi. Zifuatazo ni baadhi ya dondoo ambazo zinaweza kumsaidia msuluhishi wa kiislamu katika kazi yake ya kujenga muwafaka mwema katika jamii.

Kujua aina za maudhi na kero. Kero na maudhi ya kifamilia yako ya aina nyingi na yanatofautina baina ya mtu na mwengine. Maudhi haya yanaleta madhara sawa kama ni kwa muda mfupi au muda mrefu. Kutokana na hadithi ya Mtume SAW *" Hakuna madhara wala kudhuriana",* misingi ya kiislamu imebainisha kuwa madhara ni lazima yaondoshwe. Hivyo ili kuepusha madhara ni lazima maudhi na kero nazo ziondoshwe. Kero au maudhi yanaweza kuwa ya vitendo kama kupigwa, ya maneno kama kukashifiwa, ya tabia kama kudharauliwa na kadhalika.

Kujua kuwa mizozo ya kifamilia sio jambo la mtu binafsi yake tu. Mizozo, fujo, ukatili na mivutano inayotokea ndani ya familia sio jambo linalomhusu mke na mume tu ikawa wengine haliwahusu. Kila mmoja kwa nafasi yake ikiwa ya kifamilia, kidini, kiujirani au vyenginevyo vyovyote inampasa alishughulikie kwa kadiri ya uwezo wake. Mzozo katika nyumba moja unaweza kusababisha kuvunjika kwa familia mafungamano ya koo au ya jamii nzima ya kiislamu. Angalia uangalizi wa watoto kwa watu waliotengana, zingatia yanayotokezea kwa wajane wadogo wasioweza kujikimu baada ya kukatishwa masomo na wakawa hawana kipato wala uangalizi wa kuwatosheleza wao na watoto wao. Uislamu

unatutaka tusaidie haya kila mtu kwa nafasi yake na uwezo wake na hekma ni kujaribu kuyazuia kabla ya kutokea.

Mtume SAW anasemayo *"Mnusuru ndugu yako akiwa ni dhalimu au mwenye kudhulumiwa".* Tusiwasaidie wale tunaowaona kuwa wamedhulumiwa tu sawa kama ni mke, mume, mtoto, mfanyakazi, mzee na kadhalika ; bali wajibu wetu pia ni kumsaidia aliedhulumu ili kumuweka katika tabia na maumbile ya kibinadamu ambayo hayadhulumu. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika hadithi kudusiy "*Hakika mimi nimeharamisha dhulma juu ya nafsi yangu na nikaijaalia baina yenu kuwa ni haramu basi msidhulumiane".*

Ikabili mizozo ya kifamilia kama matatizo mengine ya kijamii. Unaposhughulikia matatizo ya wanandoa jitahidi kuwaongoza ili waweze kujua tatizo lililopo na kulitatua na sio kutoa vitisho vya ukali wako au hukmu za kwenda motoni kwa yule anaemdhulumu mwenzake. Kumbuka kuwa mtu yeyote anaweza kubadilika iwapo mbinu bora za kumuelimisha na kumkinaisha abadiklike zitafuatwa.

Tambua huduma nyenginezo zinazotolewa katika jamii. Msuluhishi anapaswa kuelewa sehemu nyenginezo za karibu ambazo pia hutoa huduma ya kusuluhisha. Sehemu hizi zinaweza kuwa ni watu wachamungu, wenye elimu na hekima; Asasi na Jumuia za kiraia au taaasisi za serikali kamavile Ofisi ya Mufti ns Mahkama za Kadhi.

Kutambua matatizo ya kijamii na kupanga mikakati ya kuishughuliki Mshauri anatakiwa ajue matatizo yaliyomo katika jamii yake ili aweze kutoa ushauri na maelekezo yaliyojengeka kwa khibra na utambuzi yakinifu. Aidha ni vyema akaitanabahisha jamii kupitia khutba na vikao vyenginevyo na kuwapa mbinu za kuyaepuka au/na kukabili matatizo hayo na kujiweka karibu na watu ili waweze kumfika kwa kuwapa ushauri, kumpatia taarifa mpya na kadhalika.

Kuomba Dua. Mtume SAW anasema *" Hakuna kinachorejesha kilichokadiriwa isipokuwa dua"* hivyo mshauri ni vyema akamuomba mungu kumfanikishia kazi yake na kuwaondoshea matatizo wote anaowashughulikia.

Tujitahidini kuchunga familia zetu na za wanajamii wenzetu ili jamii yetu iwe bora na yenye ustawi mwema. Wabillah tawfik.